SHULE YA SEKONDARI MBALAMAZIWA,
S.L.P. 128,
MAFINGA
IRINGA.
Barua pepe: mbalamaziwasecondary@gmail.com JUNE 2022

Namba za simu.
Mkuu wa shule:0766347176
Makamu mkuu wa shule: 0756518094/0757395068
Mhasibu wa shule: 0759923629
Simu ya shule: 0766518188
MZAZI WA ----------
S.L.P. ---------- ----------

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBALAMAZIWA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2022/2023KIDATO CHA TANO

Nafurahi kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano (V) katika shule hii mwaka 2022/2023 tahasusi ya:

PCB CBG

Shule ya Sekondari Mbalamaziwa ipo umbali wa kilometa sitini (60) kusini mwa mji wa Mafinga. Usafiri wa basi kutoka mjini Mafinga unapatikana katika kituo cha mabasi Mafinga magari ya kwenda Njombe au Mbeya kwa nauli ya shilingi 2,500/= (Elfu mbili na mia tano tu) hadi Mbalamaziwa shuleni. Pia kama unatoka Makambako usafiri utaupata katika kituo cha mabasi Makambako magari ya kwenda Mafinga au Iringa kwa nauli ya shillingi 2,000/= hadi Mbalamaziwa shuleni. Unaweza kuchukua usafiri wa pikipiki kutoka kituo cha mabasi Mbalamaziwa hadi shuleni kwa gharama ya shilingi 1,000/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 5/9/2022. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 4/9/2022.Mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/9/2022

1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.1 Sare ya shule.

**a) i) Sketi ndefu rangi light blue mbili (02) zenye mshono wa rinda box.
ii) Mashati meupe mikono mirefu mawili (02)
iii) Tai ndefu rangi light blue mbili (02)
iv) Makoti ya rangi ya light blue mawili mbili (02)
v) Soksi jozi mbili (02) (Stockings)

b) Nguo ya kushindia (Shamba dress) mbili rangi ya kahawia.
c) Kwa waislamu washone vazi la nusu kanzu nyeupe, Hijab (kijuba) nyeupe inayoishia chini ya kifua
d) Track suit mbili(02), light blue moja (01) na dark blue moja zenye mikanda /michirizi myeupe. Sketi fupi (nap round) ya blue ,T-shirt nyeupe, Raba nyeupe na Soksi nyeupe.

e) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi. (Zingatia Sana).

f) Poolneck nyeupe na majaketi mawili (02) meusi kwa ajili ya baridi hasa wakati wa usiku.

ZINGATIA

1. Katika kukamilisha sare ya shule, nywele lazima ziwe fupi za kuchana,kucha ziwe fupi na zisipakwe rangi na uvaaji wa mapambo ni marufuku.

1.2 Ada na michango ya shule.

a) Ada ya shule kwa mwaka ni T. Sh 70,000/= Unaweza kulipa karo yote kwa wakati mmoja aunusu (T.Sh.35,000/=) kwa muhula. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunt ya shule namba. 60201200098 Benki ya NMB Jina la Account ni Mbalamaziwa Secondary School. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye ("pay in slip") na uwasilishe shuleni.

b) Michango mingine anayotakiwa kulipa mzazi.

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani za shule kwa mwaka.

ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.

iii. Tshs.2000 kwa ajili ya nembo ya shule

iv. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya Taaluma kwa mwaka.

v.Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kulipa wapishi, walinzi,na vibarua wengine kwa mwaka.

vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na bima ya afya.

vii. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya tahadhari kwa mwaka (haitarejeshwa).

viii. Tshs 20,000 kwa ajili ya Mtihani wa mock

Jumla kuu ya michango yote kwa mwanafunzi wa bweni ni Tshs:108,000/-

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunt ya shule namba. 60201200098 Benki ya NMB Jina la Account ni Mbalamaziwa Secondary School. Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye ("pay in slip").

Gharama za matibabu zaidi ya zile zilizochangiwa shuleni zitalipwa na mzazi.

Kumbuka.

Shule itafunguliwa tarehe 5/9/2022, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo ya kufungua. Kama atakuwa hajaripoti shuleni hadi kufikia tarehe 16/9/2022 atahesabiwa kuwa ameikataa nafasi hiyo, hivyo nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine.

Hakikisha unatimiza mahitaji yote ili kuepuka usumbufu usio wa lazima na kulipa fedha benki.

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni: -

i. Cheti cha matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne/result slip

ii. Fomu za kujiunga na shule zilizojazwa kikamilifu

iii. Cheti cha kuzaliwa

iv.Vitabu vya masomo ya tahasusi yake (orodha imeambatanishwa)

v. Scientific calculator

vi.Madaftari ya kutosha kwa masomo yake/counterbook kumi (10),
mathematical set, graph pads, kalamu na vifaa vingine vya kujifunzia.

vii. Begi la kuwekea vifaa vya darasani

viii. Vyombo vya chakula(sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
Vyombo vya plastiki haviruhusiwi, inashauriwa kununua vyombo vya mfupa.

ix.Jembe na kwanja

x. Godoro futi 2.5 kwa 6
xi. Mopper moja na fagio ngumu moja
xii. Rimu moja (01) Photocopy paper size A4.
xiii. Folder File moja.
xiv. Bima ya Afya

2.0 MAHITAJI YA MALAZI YA BWENI.

i. Shuka rangi ya pink mawili (2) na foronya pink (2) na light bluu mbili na pink zake.
ii. Mablanketi mawili (2) na mto wa kulalia.
iii. Nguo za kulalia (Night Dress/pyjamas).
iv. Sanduku imara la bati pamoja na kufuli la kuhifadhia vifaa vyake maarufu kama tranka. Tunapokea sanduku moja tu.
v. Taulo moja na kanga/vitenge doti moja.
vi. Mahitaji yote ya bafu e.g. sabuni, mafuta, dawa ya meno.
vii. Ndoo moja ya kuogea na chupa ya kuhifadhia maji safi ya kunywa.
viii. Tochi 1 na betri zake/ solata moja. Itatumika endapo umeme utakatika
ix. Jacket jeusi moja kwa ajili ya baridi

Utakapofika shuleni utasomewa/utapewa sheria/kanuni za shule na utaratibu mzima wa shule hii na utalazimika kufuata. Ukikosa utaonywa na kuadhibiwa na ikilazimu utafukuzwa shule.

MWISHO, NATUMIA TENA NAFASI HII KUKUKARIBISHA HAPA SHULENI "MBALAMAZIWA SEKONDARI" NA NI MATARAJIO YANGU KUWA UFIKAPO HAPA UTATUMIAVEMA FURSA HII ULIYOTUNUKIWA NA TAIFA.

Kumbuka:-
Kama hujaripoti shuleni hadi ifikapo tarehe 16/9/2022 utahesabiwa kuwa umeikataa nafasi hii, hivyo itachukuliwa na mwanafunzi mwingine. Hakikisha unatimiza mahitaji yote kuepuka usumbufu usio wa lazima na kulipia fedha Benki.

3.0 MUHIMU KWA WANAJUMUIYA YA MBALAMAZIWA SEKONDARI.

Wanafunzi wote lazima wafuate sheria za NCHI na za shule kwa ujumla.

Lengo la sheria za shule yetu ni kumjenga mwanafunzi kuwa na mwenendo mzuri kitabia hivyo kumwezesha kufanikiwa kupata kile anachostahili hasa Taaluma. Sheria hizi zitasaidia kuleta hali ya AMANI, UMOJA na FURAHA shuleni na kumfanya kuwa raia mwema. Kila mwanafunzi aje na nia ya KUSOMA KWA BIDII, KUJITUMA na ajitahidi kuishi vizuri katika jumuiya ya shule hii na majirani zetu.

Kwa upande wa shule sisi WALIMU pamoja na WAFANYAKAZI WASIO WALIMU tutajitahidi kuishi, kumfundisha na kumlea mtoto katika maadili mema lakini tutashindwa katika kazi hii bila ushirikiano mzuri wa wazazi/walezi.

Kila mtu anatakiwa Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa"Coat of Arms" wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.

Lugha inayotumika darasani na nje ya darasa ni Kiingereza tu. Hii inasaidia kuleta ufanisi katika masomo.

Kwa vile shule ni mahali pa kusoma inatakiwa pawe na ukimya hasa sehemu za madarasani sehemu nyingine za kujifunzia.

na Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyompasa kama Ratiba ya Shule inavyoonesha. Kazi za mikono ni sehemu ya elimu inayotolewa hapa shuleni. Kila mmoja lazima ashiriki kikamilifu bila utegaji.

4.0 SHERIA ZA SHULE

A) MAHUDHURIO

Kuthamini muda wa kuwepo mahali unapotakiwa kwa mujibu wa ratiba au maelekezo kutoka kwenye uongozi wa shule

1. Kuwahi kufika shuleni na kuwepo mstarini kwa muda uliopangwa
2. Kuhudhuria shuleni kwa muda wote wa masomo
3. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
4. Kuhudhuria kazi zote za mikono na michezo
5. kuhudhuria mikutano ya shule (mfano balaza la shule,vikao vya madarasa na vikundi mbali mbali vinavyotambulika kisheria (mfano vilabu vya masomo (subject clubs), dini n.k.
6. Kuitikia miito ya dharura mara moja.

B.HESHIMA

i. Kuwathamini na kuwaheshimu wanajumuiya wote bila kuangalia umri wao
ii. kusimama na kumsalimu mwalimu yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo
iii. Kutumia kauli nzuri wakati wote
iv. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi
v. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
vi. Kuitika na kukimbilia aliko mkuu aliyekuita
vii. Kuheshimu bendera ya taifa, picha ya viongozi wa vyama na Nembo ya Taifa
viii. Kuheshimu taratibu za mikutano, Ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.
ix. Kukaa kimya darasani na kutoka nje kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyekuwepo darasani.
x. Kusimama kwenye mstari wakati wa kupokea huduma.
xi. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani au nje ya shule.
xii. Baadhi ya tabia ambazo haziruhusiwi kwa mwanafunzi ni kama zifuatazo.
    a) Kuvuta sigara, kutumia madawa ya kulevya, pombe n.k
    b) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu, kupaka rangi kucha,wanja kujichubua
    c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima au yasiyokubalika
    d) Kugombana , kutukanana, kupigana n.k
    e) Uasherati, wizi, utapeli n.k
    f) Kuvaa nguo fupi, au nguo za kubana zenye kuonesha maumbile.

C: SARE

Unapaswa kuwa na sare za shule kwa mshono unaokubalika na kwa wakati kama utakavyopangiwa kwa

i) Wakati wa masomo darasani
ii) Safari zote za nje kwa jina la Shule
iii) Wakati wa kwenda Hospitali
iv) Wakati wa mashindano

v) Unatakiwa kuwa na nguo za michezo na vazi la kazi za mikono, gauni kama utakavyoelekezwa.

D: MIPAKA YA SHULE
i) Unapaswa kufahamu mipaka ya Shule na kutokutoka nje ya mipaka hiyo bila kibali maalumu, baada ya kufika shuleni.
ii) Kibali maalumu cha kutolea ruhusa kitatolewa na mwalimu wa zamu au walimu wa malezi.
iii) Wanafunzi wasitembelee Nyumba za walimu na wafanya kazi wasio walimu, Ofisi za shule, maabara, n.k bila kibali cha wahusika mathalani mwalimu wa zamu.
iv) Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kutembelea, vilabu vya pombe, majumba ya starehe au nyumba za kufikia wageni.

E: MAGONJWA
i) Wagonjwa wote watapata kibali cha kwenda Hospitali kupitia ofisi ya malezi au tabibu wa afya (clinical officer)
ii) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa za aina yoyote. Mwanafunzi anapolazimika kuwa na dawa atoe taarifa kwa matroni ili aweze kuhifadhiwa. Wanafunzi hawaruhusiwi kupeana dawa bwenini.

F: USAFI
Usafi ni jukumu la kila mwanafunzi kama sehemu ya Maisha yake ya kila siku, hivyo atashughulikia: -
a) Usafi binafsi wa mwili na mavazi yeke.
b) Usafi wa maeneo yafuatayo kama itakavyopangwa, ukumbi wa chakula, mabweni, vyoo, madarasa, maabara, viwanja na barabara.
c) Vyakula viliwe ndani ya bwalo la chakula tu.

G: MAANDALIZI YA KUBORESHA TAALUMA
Kila mwanafunzi ajiandae kitaaluma (sambamba tahasusi za masomo) na kuwa na mahitaji muhimu ya darasani kama; Daftari (counter books10), kalamu, scientific calculator, mathematical set, na ni vizuri pia kama ataweza kupata vitabu vya kumsaidia katika masomo yake. Vitabu muhimu kwa kila somo vimeorozeshwa na kuambatanishwa na maelezo hayo.

H: MATUMIZI YA UTUNZAJI WA MALI YA SHULE NA MAZINGIRA
a) Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia na kutunza mali ya shule kama vile; majengo, viti, meza, madawati, majembe, ndoo, vitabu, vifaa vya maabara, n.k.
b) Hakikisha kwamba taa za umeme zimezimwa wakati wote mchana
c) Kisima cha maji kifunikwe baada ya matumizi
d) Weka mazingira ya Shule kuwa safi ya kuvutia. Okota karatasi na uchafu wote. Pita kwenye njia za miguu, usikatishe katishe ovyo na kukanyaga maua au majani yaliyooteshawa.

I: UTORO
Mwanafunzi ambaye hatahudhuria Shuleni bila taarifa atahesabiwa kuwa ni mtoro. Taarifa kuhusu mwanafunzi asiyehudhuria Shuleni kutokana na matatizo yoyote lazima ziwasilishwe Shuleni siku hiyo ya matatizo kwa mwalimu wa zamu au walimu wa malezi na mzazi/mlezi anayetambuliwa na shule kulingana na fomu za usajili.

J: MENGINEYO

5.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi.

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro. iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo. iv.Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.

vi. Kusuka nywele kwa mtindo wowote ule. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya. viii. Uvutaji wa sigara.

ix.Uasherati, uhusiano wa jinsia moja na kuolewa. x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.

xi.Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

xii.Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni. xiii.Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

xiv.Kudharau Bendera ya Taifa. xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

xvi. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

6.0 VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU.

a) Fomu ya utii na tabia njema kwa mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai n.k

b) Fomu ya mzazi/mlezi Historia na kukiri kukubaliana na sheria, kanuni za shule,kulipa Ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

c) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali.

d) Picha nne za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pale itakapohitajika pamoja na namba zao za simu.

TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA MBALAMAZIWA SEKONDARI.

Saini ya Mkuu wa Shule.....

Jina la Mkuu wa Shule .....

Mhuri wa Mkuu wa Shule

SHULE YA SEKONDARI MBALAMAZIWA

FOMU YA UTII NA TABIA NJEMA

Mimi ---------- (Jina kamili la mwanafunzi)

Kidato cha ---------- mwaka ----------

Natambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi na naahidi kwamba: -

a) Nitatii na kuwaheshimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya darasa, viranja, walimu, watumishi wote hadi Mkuu wa Shule.
b) Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
c) Sitashiriki katika mgomo, Fujo na makosa ya jinai.
d) Sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali maalumu kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe. e) Kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali ichukuliwe dhidi yangu ambayoni pamoja na kusimamishwa masomo ama kufukuzwa shule.

Tarehe_____ Jina na Sahihi ya Mwanafunzi……..

Tarehe _____Jina la Mzazi/Mlezi…….

Sahihi ya Mkuu wa Shule :……..

SHULE YA SEKONDARI MBALAMAZIWA

FOMU YA TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Baba ---------- Kazi yake----------
   Anwani ya mahali pa kazi ya baba ---------- Nambari ya simu ----------

2. Jina kamili la Mama ---------- Kazi yake

Anwani ya mahali pa kazi ya mama ----------Nambari ya simu ----------

3. Jina kamili la Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)
---------- Kazi na
Anwani yaMzazi/ Mlezi ---------- ----------
----
4. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto) au 'Place of Domicile'
Kijiji/Mtaa ---------- Wilaya ---------- Kata --------
---------- Mkoa ----------
Tarafa ----------
5. Mtoto anaishi na (i) Baba tu (ii) Mama tu (iii) Wazazi wote (iv) Walezi *Kata isiyohusika*
6. Dini ya Baba ---------- Dhehebu ---------- Dini ya Mama ---------- Dhehebu ---------- Dhehebu unalotaka mwanao alelewe ----------
7. Mahali na Anwani kamili ya nyumbani ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo:

Mimi ---------- (Baba/Mama/Mlezi wa ----------
Nimesoma na kuelewa sheria na kanuni za shule. Nakubali kulipa Ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

Tarehe ----------

Jina na sahihi ya Mzazi/Mlezi……..

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI MBALAMAZIWA
FOMU YA KUKUBALI (FOMU HII IRUDISHWE SHULENI)

1. Mimi ……..mwanafunzi wa kidato cha ……. nimekubali kujiunga na shule ya Sekondari Mbalamaziwa nikiwa mwanafunzi wa bweni.
2. Ninakubali masharti yote, nina ahidi kufuata sharia zote za shule.
3. Niko tayari uongozi wa shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi endapo nitakiuka masharti yaliyomo.
4. Sahihi ya mwanafunzi……., tarehe…….

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

1. Mimi…… ninakubali mtoto wangu……. wa kidato cha …… mwaka…….. kujiunga na sekondari ya Mbalamaziwa kuanzia……. tarehe ……akiwa mwanafunzi wa bweni.
2. Ninakubali masharti yaliyomo katika kujiunga na bweni ikiwa ni pamoja na kulipa karo yote ya shule na kumtimizia mahitaji mengine ya shule.
3. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa na afya isiyoridhisha ambayo itahitaji ukaribu wa matunzo ya mzazi/mlezi mwenyewe.
4. a) Anuani yangu ya kudumu ni ……..

   b) Jina na anuani ya mlezi wa karibu mjini Iringa ambaye shule inaweza kuwasiliana naye katika matatizo mbali mbali yam toto ni…….
5. Saini ya mzazi/mlezi……terehe……..

SHULE YA SEKONDARI MBALAMAZIWA
FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI

1. Jina kamili……
2. Mahali ulipozaliwa……..
3. Tarehe ya kuzaliwa …….
4. Uraia…….
5. Anuani ya nyumbani……
6. Jina la mzazi/mlezi……..
7. Anuani ya mzazi/mlezi (kama tofauti na hiyo hapo juu)…….
8. Ndugu wa karibu.Anuani yake, kitongoji/mtaa……

NA	JINA	UHUSIANO	ANUANI	SIMU
1				
2				
3				
4				

9. Dini……
10. Kidato alichopokelewa……

11. Shule uliyotoka……
12. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba n.k…….
13.Wilaya unakotoka……mtaa……kata……
14.Saini ya mwanafunzi……. tarehe……..
15.Saini ya mzazi/mlezi…….tarehe…….

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MBALAMAZIWA

MASHARTI YA KUJIUNGA NA BWENI
Pamoja na sharia na kanuni muhimu za shule unapaswa
1. Kukubaliana na sharia na kanuni zote za shule
2. Kufuata ratiba ya siku kwa mwanafunzi wa bweni
3.Kuhudhuria roll-calls zote kama inavyopangwa na walezi
4. Kuhudhuria "Preps" na vipindi vyote vya darasani
5. Kuishi kwa amani, upendo, na ushirikiano wa kidugu na wanajumuiya wote
6. Kula "Menyu" moja iliyoandaliwa na shule bila kuleta usumbufu wa kujichagulia chakula.
7. Kuchangia gharama za matengenezo ya uharibifu wowote inapolazimu.
8. Kutomleta au kumwagiza mgeni yoyote ndani ya bweni. (mwanafunzi wa kutwa ni miongoni mwao).
9.Kutoleta wageni au kukaa ndani ya bweni bila ruhusa ya walezi wakati wa masomo.
10. Hairuhusiwi kupika chochote
11. Ni marufuku kwa wanafunzi wavulana kuingia bweni la wasichana
12. Hairuhusiwi kulala nje ya shule bila ruhusa ya mkuu wa shule.
13.Hairuhusiwi Kutoka nje ya shule bila kibali maalum kwa utawala
14.Kuvaa sare ya shule wakati wote wa vipindi na awapo nje ya mipaka ya shule (kwa shughuli binafsi,shule au dini).

7.0. VITABU

Ifuatayo ni baadhi ya orodha ya vitabu vinavyotumika darasani. Wanafunzi wajitahidi kuwanavyo angalau vichache.

CHEMISTRY:

i. Conceptual chemistry XI and XII - By S. Chand ii. Inorganic Chemistry - By Ngaiza iii. Advanced Inorganic Chemistry - Vol I and II -By chand iv. Organic Chemistry Part A By Tanzania Publishing House
v. Organic Chemistry Part B By Tanzania Publishing House vi. Physical Chemistry - By S.Chand vii. Advanced Chemistry - By Cambridge low price Edition Philip Mathew. viii. A level Chemistry - 4th Edition EN Ramsiden ix. Practical Chemistry - By Mlungu.

PHYSICS:

i. A' level physics 4th edition. By Roger Muncaster ii. S. Chand's principle of physics for class xi iii. S. Chand's principle of physics for class xii iv. Nelkon & Parker 7th edn v. University physics vi.

Calculation for A' level physics vii. Engineering physics c.

BIOLOGY:

i. CJ CLEGG with DG MACKEAN (2000) Advanced Biology principles and Application 2nd Ed, Hodder Murray London ii. Sylvia S Mader (1996), Biology (5th Ed) Wm C. Brown publisher London

iii. DJ Taylor et al (1997), BIOLOGICAL SCIENCE, Cambridge University press - New York.

iv. MBV Roberts (1986), Biology A functional Approach (4th Ed)

v. Ann Fullick et al (2011), A level Biology, students Book, Longman.

GENERAL STUDIES

i. General studies for A' level certificate form v by. RICHARD R MBALASE

ii. General studies for A' level certificate form vi. By RICHARD R. MBALASE

GEOGRAPHY:

i. Practical geography Alive by Zisti - Map Reading, photography Interpretation, Field Research, Statistics, and Survey Illustrated by Ellias Anthony Mkoko - Affordable Edition for secondary and High school learners kot publishers

ii. A comprehensive approach to physical geography by D.T. Msabila

iii. Human and Economical Geography by Gillan C. Morgan

iv. Soil and Climatology by Zisti

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MUFINDI DISTRICT COUNCIL.

MBALAMAZIWA SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by medical officers in a recognize Hospital in respect of all new entrants to Mbalamaziwa Secondary School).

Student Full name.....

Age..... years Sex……

1. Blood count (Red&White).....
2. Urine examination.....
3. Stool examination.....
4. Syphilis and other Venereal diseases Test.....
5. T.B test.....
6. Ear test.....
7. Eye test.....
8. Speen.....
9. Abdominal.....
10. Test for pregnancy (for girls only)

……

10. Additional information or any other physical, hereditary or infectious disease:

Treatment after examination:

……

MEDICAL CERTIFICATE:

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue for further education.

Signature .....

Designation.....

Station..... (Official stamp).....

Date.....

(NB: Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika na Serikali).